



NAFASI ZA AFISA MAUZO (SABASABA)

Kampuni ya Heritage Drinking Water Limited (HDWL) ilianzishwa April 7, 2020. HDWL inachakata na kuuza maji safi na salama ya kunywa kwa kiwango cha TBS kwa bei nafuu sana mkoani Dar es Salaam ili ku-*Okoa Pesa na kuu-Tunza Mazingira*. Kampuni inatangaza nafasi 52 za afisa mauzo kwa ajili ya Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (sabasaba) kuanzia 28 Juni hadi 13 Julai 2024. Kama una sifa tafadhalii tuma faili moja la PDF la maombi yako yote kwenye namba hii +255 656 000 678 kwa njia ya WhatsApp.

SIFA ZA MWOMBaji

- Awe anajitambua na kujielewa
- Awe mchangamfu na mwenye tabasamu kwa wateja
- Awe shapu sana kuhudumia wateja wengi
- Awe na lugha nzuri kwa wateja na mvumilivu kwa wateja
- Awe mwaminifu kwenye pesa za mauzo ya siku ya kampuni
- Awe na uwezo wa kuhudumia wateja akiwa amesimama kwa mda mrefu
- Elimu: kidato cha nne na kuendelea.

Mwisho wa kutuma maombi: 20 Juni 2024

Viambatanisho vya maombi vifuatavyo vitumwe kama PDF faili moja kwenda +255656000678 kwa njia ya WhatsApp:

1. Wasifu/ CV;
2. Barua ya maombi ya mkono;
3. Barua ya mtendaji wa mtaa au kopi ya kitambulisho cha NIDA;
4. Barua ya mdhamini yenye picha ya mdhamini na kopi ya kitambulisho chake;
5. Pasipoti saizi mbili; na,
6. Kielelezo kuwa ana simu janja/ smartphone.

Anuani ya barua:

P.O. BOX 55150, Dar Es Salaam, Tanzania, Changanyikeni Street, Shina No. 5, Block 40.

Simu ya kampuni kwa maulizo mengine na jinsi ya kufika HQ: +255 656 000 678

Tarehe muhimu:

Usaili wa kwanza: Ijumaa 21 Juni 2024.

Mafunzo ya RO: Jumamosi 22 Juni 2024 (kuna ada ya mafunzo ya RO ya 10,000)

Usaili wa pili: Jumatatu 24 Juni 2024

Maelekezo ya kazi: Jumanne 25 Juni 2023

Kuanza kazi: Alhamisi 27 Juni 2024.